TOLEO NO. 01
JANUARI - JANUARI 2022

# OMKR Zanzibar

KWA MAENDELEO YA WANANCHI WA ZANZIBAR

ISSN NO. 01

## Mhe. Othman ahimiza juhudi za pamoja kurejesha Z'bar ya kijani

Habari Uk. 10



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi amemuapisha Othman Masoud Othman Sharif kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar kufuatia uteuzi alioufanya Machi 01, 2021.*

# Ifahamu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Z'bar

Habari Uk. 6

## Bodi ya Wahariri

**Mhariri Mkuu:**
Dkt. Omar D. Shajak

**Msaidizi Mhariri:**
Daima M. Mkalimoto

**Mhariri Msanifu:**
Yussuf A. Hassan

**Msaidizi Msanifu:**
Masoud Kassim Abass

**Wajumbe:**
Sabra Ali Mohammed
Rashid Omar Kombo
Raya Hamad Suleiman
Said Mussa Muhammed

## Wasiliana nasi kwa:

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais
**S.L.P**: 2808
**Migombani -Zanzibar**
**Simu:** +255 (24) 2232475
**Barua pepe:** Info@omkr.go.tz
**Tovuti:** www.omkr.go.tz




# SALAMU ZA MHE. WAZIRI WA NCHI OMKR



**Mhe Harusi Said Suleiman**
**Waziri wa Nchi OMKR Zanzibar.**

OFISI ya Makamu wa Kwanza wa Rais inashughulikia Idara na Taasisi mtambuka, na kwamba shughuli za Idara na Taasisi hizo moja kwa moja zinahusiana na maisha ya kila siku ya wananchi wa Zanzibar.

Kutokana na umuhimu wa majukumu ya taasisi hizo kwa wananchi wa Zanzibar, tumeamua kuanzisha jarida hili, ambalo lengo lake ni kuwapatia elimu wananchi kwa undani kuhusu namna taasisi hizo zinavyotekeleza majukumu yake.

Miongoni mwa majukumu ya msingi yaliyopo katika Ofisi hii ni pamoja na kupambana na athari za janga la maradhi ya UKIMWI, ambapo kwa zaidi ya miaka 40 tangu ulipogunduliwa ugonjwa huo haujapata dawa wala chanjo hadi sasa.

Kwa kipindi chote hicho cha kugunduliwa tatizo hili la UKIMWI tayari umeondosha maelefu ya ndugu, jamaa, watoto na wapendwa wetu, hivyo Ofisi hii inawajibika kuhakikisha mikakati thabiti inawekwa ili kuzuia kasi ya maambikizi mapya ya maradhi haya.

Kwa upande mwengine tatizo la Mazingira nalo lipo Zanzibar kutokana na ukweli kwamba dunia inakabiliwa na janga la athari za mabadiliko ya tabianchi. Hali hiyo inatokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa gesi zinazoongeza hali ya joto duniani.

Zanzibar kama sehemu ya dunia, imeanza kushuhudia athari za mabadiliko ya Tabianchi inayotokana na athari za tatizo hilo, tayari yapo maeneo kadhaa ya Unguja na Pemba, kina cha bahari kimeongezeka na kusababisha athari za mawimbi kumongonyoa fukwe huku kima cha bahari kupanda juu.

Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu ni taasisi nyengine ambayo ipo chini ya Ofisi yangu. Hakuna asiyeelewa changamoto zinazowakabili wenzetu hawa katika jamii ikiwemo kukosa fursa mbalimbali na hata kujikuta wakinyanyapaliwa na kusababisha wakati mwengine jamii zao kuwaficha.

Ofisi yetu inajukumu la msingi la kusimamia sera na sheria za ndani ya nchi yetu pamoja na mikataba ya kimataifa ili kuhakikisha Watu wenye Ulemavu wanaondokana na changamoto zinazowakabili.

Dawa za kulevya ni janga jengine ambalo linawaathiri sana vijana, ambao ndio nguvu kazi ya uzalishaji katika nchi yoyote. Zanzibar inakadiriwa kuwa watumiaji wa dawa za kulevya wanaofikia 10,000. Watumiaji wa dawa hizo wanakabiliwa na athari nyingi zikiwemo kujihusisha na uhalifu, matatizo ya kiafya na kadhalika.

Tunakukaribisheni kulisoma jarida hilo ambalo limesheheni taarifa za uhakika juu ya namna Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia Ofisi hii, inavyotekeleza mipango na mikakati mbali mbali ya sekta hizo mtambuka kwa ajili ya kustawisha maisha ya wananchi wa Zanzibar.

Sina shaka taarifa mbalimbali zilizomo kwenye jarida hili zitachangia kuongeza elimu, uelewa, ufahamu na maarifa kwa jamii na kusaidia wananchi wengi kuelewa namna serikali ilivyojidhatiti kuwapatia huduma wananchi wake.

Kwa mnasaba huo basi tunaomba wananchi kuunga mkono juhudi za serikali katika kukabiliana na masuala yote yanayoathri jamii yetu kwa kuhakikisha kwamba wanafuata miongozo, taratibu na sharia pamoja na wao wenyewe kuwa sehemu ya mapambano mbali mbali yanayoathiri mustakabali wa taifa.

## Maoni ya Mhariri

# Kuanzishwa Jarida la Ofisi ya Makamu iwe chachu ya uwajibikaji kwa wote



**Dk. Omar Dadi Shajak**
**Katibu Mkuu OMKR Zanzibar.**

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, kwa mara ya kwanza imeanzisha Jarida lake litakalotolewa kila baada ya miezi sita. Malengo makuu ya Jarida hili ni kuchapisha na kutoa taarifa zinazohusu masuala mbali mbali juu ya utekelezaji wa mipango, sera, sheria na mikakati mbali mbali kuhusu usimamizi wa ofisi hii na taasisi zake zote.

Sisi tunaamini kwamba suala la kuanzisha jarida hili ni miongoni mwa jambo muhimu na itakuwa nyenzo bora ya kusaidia kupatikana taarifa na kutoa uelewa kwa jamii na taifa kwa jumla juu ya masuala muhimu yanayohusu sera na mipango ya Ofisi hii na Serikali pamoja na utekelezaji wake unavyofanyika hatua kwa hatua.

Aidha tunaamini kwamba Jarida linalenga kusaidia kupima na kuweza kufahamu kiwango cha ufanisi kilichofikiwa iwapo malengo yaliyowekwa yanatimia na pia kuona changamoto zilizojitokeza na jitihada zinazofanyika kuzikabili hatua kwa hatua.

Hapana shaka kuelekeza nguvu za pamoja ni jambo jema kwani mambo yalivyopangwa yanaweza kuwa na matokeo chanya kutimiza dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kutoa huduma kwa umma kwa lengo la kuchangia maendeleo ya Zanzibar kuwa endelevu.

Hivyo basi tunapongeza uamuzi wa Ofisi kuona kuna haja kubwa ya kutenga bajeti kwa ajili ya kazi za utayarishaji wa jarida pamoja na uchapaji na hatimaye kuweza kuwafikia wadau mbali mbali na kupata taarifa sahihi zilizo kamilifu za utekelezaji wa mambo ya msingi ndani ya Ofisi kupitia taasisi zake zote.

Ni imani yangu kwamba jarida hili, pamoja na mambo mengine litatumika vyema na taasisi na Idara zote zilizopo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar kwa lengo la kuifanya jamii ielewe shughuli za taasisi hizo.

Kwa upande mwengine Uongozi wa Jarida hili unaahidi kufanya kazi kubwa ya kuchapisha makala za matukio pamoja na mambo muhimu ili kuonesha uwajibikaji kwa nia ya kufikia malengo ya shughuli muhimu za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na taasisi zake.

Wakuu wote wa Idara na vitengo vilivyopo chini ya Ofisi hii wahakikishe wanalitumia ipasavyo jarida hili kwa kuwasilisha makala zao mbali mbali ili zichapishwe kwenye jarida.

Hivyo ni vyema kwa pamoja kuendelea kushirikiana ili kuhakikisha kwamba jarida hili linatimiza malengo yake na kuwa endelevu na lenye tija sio tu kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, lakini pia Serikali na Taifa kwa jumla.

Mwisho tunawaomba wasomaji na wadau wetu wengine wa ndani na nje ya Ofisi kulitumia jarida hili ipasavyo, sio tu kwa kuwasilisha Makala zao na kuchapishwa, lakini pia watumie kama njia ya kutoa matangazo yao, ujumbe na taarifa mbali mbali zinazowahusu.

Tunaahidi kuwa bega kwa bega na watendaji wote wa Ofisi ikiwa ni pamoja na kuhakisha kwamba sera na miongozo ya Serikali ndio dira muhimu ya kufuatwa ili mchango wa jarida kimaendeleo uweze kupatikana.

# Mabadiliko ya tabianchi yaiathiri Zanzibar



**MABADILIKO** ya tabianchi ni mabadiliko ya mfumo na mwenendo wa hali ya hewa unaotokea kwa kipindi cha muda mrefu kuanzia miaka thelathini au zaidi. Hivi sasa nchi nyingi duniani zinakabiliwa na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi na kuwa tishio kwa ustawi wa jamii hususan kwa nchi masikini na zile za visiwa ambazo zinapambana katika kukabiliana na hali ngumu ya maisha ya watu wake na upatikanaji wa uhakika wa chakula.

Zanzibar ikiwa ni sehemu ya dunia na ambayo pia ni nchi ya kisiwa inaguswa na changamoto ambazo zinasababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Mabadiliko ya tabianchi yanaweza kusababishwa na kuwepo mabadiliko ya mifumo ya asili ya dunia ambayo yanatokea wenyewe kwa nguvu za kimaumbile ikiwemo milipuko ya volkano, joto linalosababishwa na nishati ya jua na mambo mengine.

Shughuli zinazofanywa na binadamu ambazo hazizingatii taratibu za uhifadhi wa mazingira pia zimebainika kusababisha mabadiliko ya tabianchi kama vile uzalishaji katika viwanda vikubwa hususan katika nchi zilizoendelea.

Ukataji holela wa misitu nao pia unapelekea kupungua kwa miti ambayo inasaidia kufyonza hewa ya carbondioxide, uchomaji wa mafuta katika vyombo vya usafiri, uchomaji wa taka ngumu pia ni miongoni mwa shughuli za kibinadamu zinazosababisha mabadiliko ya tabianchi.

Shughuli zinazofanywa na binadamu kila uchao bila ya kufuata taratibu husababisha kuongezeka kwa gesi joto kwenye usawa wa dunia na kuchangia kwa asilimia kubwa mabadiliko ya tabianchi. Mfano wa gesi joto ni Methane, Nitrous oxide, Perfluorocarbons, Hydrofluorocarbons, Sulphur hexafluoride, Carbondioxide, Kloroflorokaboni Nitrous oxide. Ongezeko la gesi joto linachangia sayari yetu kuwa na joto lisilo la kawaida pamoja na kuzuia miale inayoelekea angani na kutakiwa irudi katika sayari ya dunia kutoweza kurudi na kufanya kiwingu kikubwa cha gesi hizo.

Katika miaka ya hivi karibuni, hali ya hewa ya dunia imekuwa ikibadilika kwa kasi kuliko ilivyokuwa imetegemewa. Hii ni kutokana na ukweli kwamba katika kipindi cha miaka 200 iliyopita, maendeleo ya binadamu na viwanda katika nchi zilizoendelea yamesababisha mabadiliko ya haraka angani ambayo yalitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa gesi-joto zinazosababisha ongezeko la joto duniani.

Kwa mujibu wa utafiti wa athari za mabadiliko ya tabianchi kwa uchumi wa Zanzibar ambao ulifanyika mwaka 2012, imebainika kuwa Zanzibar inakabiliwa na ongezeko la kiwango cha joto, kubadilika kwa miongo ya mvua, kuongezeka kwa upepo mkali wakati wa kusi na kaskazi, ongezeko la kina cha bahari, mawimbi ya bahari pamoja na kuongezeka kwa matukio mbali mbali ya maafa yanayohusishwa na mabadiliko ya hali ya hewa. Maeneo ambayo yapo chini ya contour za mita 5 yapo hatarini zaidi kuathirika na kupanda kwa kina cha bahari.

Kwa upande wa Kisiwa cha Unguja eneo hilo ni wastani wa kilomita za mraba 328 na Pemba ni kilomita za mraba 286. Makadirio ya idadi ya watu wanaoishi katika maeneo hayo ni 224,000 sawa na asilimia 29 kwa upande wa Unguja na watu 281,000 sawa na asilimia 54 kwa Pemba.

Aidha, utafiti huo umebaini karibu sekta zote kuu za uchumi wa Zanzibar zinaathiriwa na mabadiliko ya tabianchi na kuainisha kuwa Zanzibar ina maeneo 148 - Unguja 25 na Pemba 123 - ambayo yameathirika kwa kuingiwa na maji ya bahari. Sekta za kilimo, uvuvi, utalii, maji, makaazi na miundombinu ni sekta kuu zinazoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi Zanzibar.

Katika sekta ya kilimo uzalishaji wa mazao ya kilimo umeathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na kuwepo kwa uchache wa mvua, mvua kutonyesha kwa wakati uliozoeleka na kuingia kwa maji ya bahari katika maeneo ya kilimo, hivyo kufanya maeneo yaliyokuwa yakitumika kwa kilimo kutotumika tena.

Wakulima wengi Zanzibar wanategemea kwa kiasi kikubwa kilimo cha mvua ambacho huajiri zaidi ya asilima 70 ya watu. Kwa upande mwengine uzalishaji wa mazao ya kilimo umeathiriwa na mmong'onyoko wa fukwe kunakochangiwa na kupanda kwa kina cha maji ya bahari. Sehemu mbalimbali za kilimo hapa Zanzibar, hasa Pemba, zimeathirika kutokana na kuingia kwa maji ya bahari na hivyo kufanya maeneo yaliyokuwa yakitumika kwa kilimo kutotumika tena.

Kilimo cha mwani nacho kimeathiriwa na mabadiliko ya tabianchi kutokana na ongezeko la joto na nguvu za mionzi kupenya baharini kwa kiwango kikubwa. Athari hizo zimesababisha kilimo cha mwani kuhamishiwa kwenye kina kirefu cha maji.

Sekta ya uvuvi ni miongoni mwa sekta muhimu Zanzibar na inatoa ajira kwa zaidi ya watu 49,000. Athari za mabadiliko ya tabianchi katika sekta ya uvuvi zinahusishwa zaidi na uharibifu wa matumbawe ambayo ni maeneo muhimu ya mazalio, makuzio na malisho ya samaki baharini. Asilimia 90 ya samaki wanaovuliwa Zanzibar wanaishi katika matumbawe. Ongezeko la joto la bahari hupelekea kuchubuka na kufa kwa matumbawe na hivyo husababisha samaki kuhama hasa kwenye maeneo ya karibu ambayo joto lake huwa kubwa. Hali hii hupunguza kipato cha wavuvi hususan wavuvi wadogo na hatimaye kuathiri ustawi wa maisha yao na wananchi kwa jumla.

Zanzibar inategemea maji yaliyopo

***Inaendelea Uk. 5...***

# Mabadiliko ya tabianchi yaiathiri Zanzibar

*Inatoka Uk. 4*

chini ya ardhi (groundwater) kama vile visima na chemchem kwa ajili ya matumizi mbali mbali. Maji yaliyopo chini ya ardhi yanategemea kiwango cha mvua kinachonyesha. Uhaba wa mvua zinazonyesha unaathiri kiwango cha maji ya ardhini. Baadhi ya visima ambavyo tokea enzi wananchi walikuwa wanavitumia kwa ajili ya maji ya kunywa na shughuli nyengine, hivi sasa haviwezi kutumika tena kwa shughuli hizo kutokana na kuingia maji ya bahari. Maji yaliomo kwenye chemchem na visima kadhaa katika visiwa vya Zanzibar (Unguja na Pemba) yameanza kupungua.

Katika sekta ya utalii athari ambazo zinaweza kuchochewa na mabadiliko ya tabianchi ni kule kunyesha mvua za mafuriko ambazo zinaweza kuporomosha majengo ya Mji Mkongwe ikiwa moja ya kivutio. Athari za mabadiliko ya tabianchi juu ya utalii katika visiwa hivi ni kubwa. Utalii wa visiwa hivi ni ule wa kutembelea maeneo ya Mji Mkongwe, fukwe za bahari, kuangalia matumbawe na kutembelea maeneo ya maumbile.

Kuongezeka kwa matukio ya hali mbaya ya hewa kama vile mafuriko yamesababisha uharibifu wa miundombinu ikiwa ni pamoja na barabara, viwanja vya ndege, mifumo ya mawasiliano na majengo. Kwa mfano, kipindi cha April – May, 2017 mvua kubwa ilisababisha mafuriko maeneo mbali mbali Zanzibar na kuleta uharibifu mkubwa wa barabara, madaraja, nguzo za umeme, mitaro ya maji ya mvua, mfumo wa maji safi na makaazi ya watu.
Baada ya kuona athari za mabadiliko ya tabianchi zilizojitokeza katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua hatua za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ili kuhakikisha wananchi wanaishi katika mazingia salama. Miongoni mwa hatua hizo ni kutayarisha Mkakati wa Zanzibar wa Mabadiliko ya tabianchi wa mwaka 2014 ambao unatoa dira kwa Serikali na wadau wengine juu ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kujihami na kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

Hatua nyingine ni kushirikiana na jamii kupanda miti ya mikoko ambapo kwa mujibu wa Ripoti ya Hali Halisi ya Mazingira ya 2021, jumla ya hekta 238 za mikoko zimepandwa katika maeneo ya Kisakasaka, Kilimani, Kisiwapanza, Ukele, Tovuni na Tumbe.

Hatua nyingine zilizochukuliwa ni kutoa elimu juu ya athari za mabadiliko ya tabianchi kwa jamii kupitia mikutano, redio, TV pamoja na makongamano; kufanya utafiti wa athari za kiuchumi.

## MASHAIRI

**WALEMAVU NAO WATU**

Leo nakuja na bango, Upatu kuwapigia
Wasanifu wa majengo, Wasofuata sheria
Walemavu wa viungo, Kutokuwahurumia
**Tujengapo nyumba zetu, Haya tuyazingatie**

Nyumba nyingi si rafiki, Walemavu kutumia
Huduma hazifikiki, Washindwa ngazi kukwea
Hatuwatendei haki, Zilowekwa kisheria
**Tujengapo nyumba zetu, Haya tuyazingaatie**

Hata nyumba za ibada, Baadhi kwao udhia
Kwa walemavu ni shida, Njia hawakujengewa
Hapo bila msaada, Wenzetu twawasumbua
**Tujengapo nyumba zetu, Haya tuyazingatie**

Na nyumba za biashara, Hata makaazi pia
Haitumiki busara, Hawa kuwafikiria
Jambo hili linakera, Hayupo wa kukemea
**Tujengapo nyumba zetu, Haya tuyazingatie**

Pia huduma ya vyoo, Mtihani umekuwa
Maalumu kwao wao, Havipo wanaumia
Na mafundi wajengao, Hili wanapuuzia
**Tujengapo nyumba zetu, Haya tuyazingatie**

Walemavu nao watu, Yafaa kuzingatia
Wamo miongoni mwetu, Haki wanahitajia
Hali zao dhima kwetu, Hatuna pa kukwepea
**Tujengapo nyumba zetu, Haya tuyazingatie**

Tamati hapa nafika, Ila hili tawambia
Hujafa hujaumbika, Keshoyo hujaijua
Sote tunahisabika, Walemavu tarajiwa
**Tujengapo nyumba zetu, Haya tuyazingatie**

**Mtunzi: Salum Vuai Issa.**

**TUYATUNZE MAZINGIRA**

Nianze utangulizi, Nikimuomba Mwenyezi
Nisipate bumbuwazi, Pokea na maamkizi
Lengo langu liko wazi, Ni Mazingira kuyaenzi
**Zanzibar ni Moja, Tuyatunze mazingira**

Mamlaka ya Usimamizi, Mazingira na Idara
Wao watangaza wazi, Uchafuzi ni madhara
Fuata wawelekezi, Fika ZEMA na Idara
**Zanzibar ni Moja, Tuyatunze mazingira**

Idara ya Mazingira, Elimu wanatujuza
Kuyatunza mazingira, Yasije yakatuviza
Wanafunzi wa Kwarara, Mtende Kisiwapanza
**Zanzibar ni Moja, Tuyatunze mazingira**

Uoto asili rejesha, Hewa safi twahitaji
Miti mingi kuotesha, Kuhuisha vyanzo vya maji
Mikarafuu na mikesha, Yote tunaihitaji
**Zanzibar ni Moja, Tuyatunze mazingira**

Maisha ni Mazingira, Mazingira ni maisha
Mazingira ni ajira, Utapoyaimarisha
Utalii werawera, Uchumi kuupaisha
**Zanzibar ni Moja, Tuyatunze mazingira**

Tunapojenga minara, Sikimbilie mitaji
Tathmini ya Mazingira, Kwa wale wawekezaji
Sheria pia na Sera, lazima zitawahoji
Zanzibar ni Moja, Tuyatunze mazingira

7.Awamu ya Nane imara, Ilani yatekelezwa
Wala haina masihara, Sheria kutekelezwa
Ukiyaleta madhara, Jela utakwenda lazwa
**Zanzibar ni Moja, Tuyatunze mazingira**

Mifuko ya palastiki, Ni sumu isiyooza
Aridhini inabaki, Hali inayochukiza
Visiwa vitaghariki, Sheria tukipuuza
**Zanzibar ni Moja, Tuyatunze mazingira**

Mkataba wa Kyoto, Wajibu kutekeleza
Tutahadhari na moto, Kaboni kuipunguza
Na misumeno ya moto, Inazidi kuumiza
**Zanzibar ni Moja, Tuyatunze mazingira**

Tamati shairi hili, Wasia wangu sikiza
Jamii sikia hili, Kutunza nasisitiza
Mazingira mfadhili, Iwapo tutayatunza
**Zanzibar ni Moja, Tuyatunze mazingira**

Raya Binti Mchere, Mdau wa Mazingira
Nataka tutoke sare, Tuyatunze mazingira
Zanzibar na ing'are, Na hizi ndio fikira
**Zanzibar ni moja, Tuyatunze mazingira**

**Mtunzi Raya Hamad Mchere**

# Ifahamu Ofisi ya Makamu wa Kwanza Wa Rais




***Jengo la Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais liliopo Migombani mjini Zanzibar.***

**OFISI** ya Makamu wa Kwanza wa Rais ni taasisi iliyoanzishwa rasmi mwaka 2010 kufuatia marekebisho ya 11 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, iliyoruhusu kuwepo na kuanzishwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Ibara ya 39 (5) ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 inaelekeza kuwepo Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar ambaye atakuwa Mshauri Mkuu wa Rais katika kutekeleza kazi zake.

Kimuundo Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, inaongozwa na Makamu wa Kwanza wa Rais ambaye anasaidiwa na Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Mtendaji Mkuu wa Ofisi ni Katibu Mkuu ambaye anasaidiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi kupitia wakuu wa Taasisi na Idara.

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inaongozwa na sera na sheria mbali mbali. Kwa sasa Ofisi inasimamia sera tatu na Sheria tano ambazo ndio miongozo mikuu ya kutimiza malengo yaliyowekwa.

Miongoni mwa hizo ni Sera ya Mazingira ya 2013, Sera ya Watu wenye Ulemavu ya 2018, Sera ya VVU na UKIMWI ya 2012, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namb. 3 ya 2015, Sheria ya Uanzishwaji wa Tume ya UKIMWI Namb. 3 ya 2002, Sheria ya Kusimamia na Kukinga Masuala ya UKIMWI Namb. 18 ya 2013, Sheria ya Watu wenye Ulemavu (Haki na fursa) Namb. 9 ya 2006, Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Namb. 8 ya 2021.

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inaundwa na Taasisi tatu zinazojitegemea na Idara sita ambazo ziko chini ya Ofisi Kuu moja kwa moja.

Taasisi zinazojitegemea ni Tume ya UKIMWI, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (ZEMA).

Idara zilizopo chini ya Ofisi Kuu ni Ofisi ya Faragha, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu, Idara ya Mazingira na Ofisi Kuu Pemba.

Ofisi ya Faragha ndio yenye dhamana ya kusimamia na kuhakikisha kwamba kazi na shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais zinafanyika kwa ufanisi mkubwa. Ibara ya 39 (5) ya Katiba ya Zanzibar ya 1984, Toleo la 2010, inaeleza kuwa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais ni Mshauri Mkuu wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kutekeleza kazi zake za kila siku.

Majukumu mahasusi ya Idara ya Faragha ni pamoja na kuratibu shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais ikiwemo utoaji wa huduma zote muhimu kwa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na familia yake; kumsaidia Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais katika masuala yote ya kuimarisha mahusiano na jamii; kuwa ni njia ya mawasiliano baina ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na Serikali hasa viongozi na wananchi; na kutunza makaazi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Majukumu mengine ni kupokea na kufuatilia kero, malalamiko na migogoro ya wananchi na kuyafanyia kazi kwa kushirikiana na Taasisi husika; kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa ahadi za Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais alizozitoa kwa wananchi; kuimarisha mashirikiano na mahusiano ya kitaifa na kimataifa; na kuratibu ziara za Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais za ndani na nje ya nchi.

Ofisi nyingine ni Idara ya Watu wenye Ulemavu. Idara hii itabadilika na kuwa Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu

***Inaendelea Uk. 7...***

# Ifahamu Ofisi ya Makamu wa Kwanza Wa Rais

***Inatoka Uk. 6***

baada ya kupitishwa sheria ya 2022. Shughuli za uratibu wa masuala ya Watu wenye Ulemavu zinasimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Idara hiyo. Idara hii imeundwa kwa Sheria ya Watu wenye Ulemavu ambayo ni Sheria Namb. 9 ya 2006. Idara inawajibika kusimamia na kuratibu upatikanaji wa haki na fursa kwa Watu wenye Ulemavu Zanzibar pamoja na kusimamia programu mbali mbali.

Majukumu ya Idara ni kuimarisha upatikanaji wa haki na fursa kwa Watu wenye Ulemavu; kuondosha ubaguzi dhidi ya Watu wenye Ulemavu na kupendekeza njia za kuondoa ubaguzi; kuhimiza mwenendo mzuri katika kuwashughulikia Watu wenye Ulemavu; kuunganisha sera na mipango inayohusu Watu wenye Ulemavu; kusimamia na kutathmini mipango na shughuli za Watu wenye Ulemavu; kutoa elimu na ujuzi kwa Watu wenye Ulemavu ili kuwawezesha kujitegemea; na kuanzisha, kutunza na kukuza taarifa za Watu wenye Ulemavu na taasisi zao kwa lengo la kuwasajili Watu wote wenye Ulemavu.

Majukumu mingine ya Idara ni pamoja na kuweka mpango maalum wa elimu isiyo rasmi kwa Watu wenye Ulemavu wa aina zote, na kwa hali itakavyowezekana kuanzisha maandishi ya nukta nundu na maktaba za kurikodia kanda kwa watu wasioona; kufanya upelelezi na kutoa mapendekezo ya malalamiko yeyote yanayotolewa chini ya Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Namb. 9 ya 2006; kupendekeza misamaha na afueni kwa Serikali kwenye masuala yanayohusu Watu wenye Ulemavu; kutoa taarifa za kila mwaka kwa mujibu wa kifungu cha 37 cha Sheria Namb. 9 ya 2006; na kutafuta rasilimali za mfuko au kutafuta fedha kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu.

Tume ya UKIMWI ni taasisi nyingine iliyoko chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Tume imeanzishwa kwa Sheria Namb. 3 ya 2002. Uratibu wa masuala ya UKIMWI unasimamiwa na Sheria hii pamoja na Sheria ya UKIMWI Namb. 18 ya 2013. Kwa mujibu wa ripoti ya utekelezaji ya Julai - Disemba 2021, hadi kufikia Juni 2021, Zanzibar inakadiriwa kuwa na watu 8,147 wanaoishi na virusi vya UKIMWI ambapo wanawake ni 5,621 na wanaume 2,526.

Majukumu ya Tume ya UKIMWI ni pamoja na kudhibiti na kupunguza madhara ya janga la VVU/UKIMWI pamoja na kuratibu utekelezaji wa mikakati ya sera ya UKIMWI; kuhamasisha na kusimamia rasilimali, kwa mwitikio wa kitaifa wa kupambana na VVU na UKIMWI; kukuza uwezo wa sekta mbali mbali za jamii ili kukabiliana na janga la VVU/UKIMWI pamoja na kuratibu maoni yao.

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pia inaongoza Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar. Taasisi hii inaongozwa na Kamishna Mkuu. Katika kuimarisha jitihada za kupambana na Dawa za Kulevya, Serikali imeanzisha Mamlaka hii kwa Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Namb. 8 ya 2021.

Miongoni mwa majukumu ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar ni kuchunguza makosa ya dawa za kulevya na makosa mengine yanayohusiana nayo; kuchukua hatua za kudhibiti na kupambana na usafirishaji wa dawa za kulevya; kuanzisha na kuimarisha mashirikiano kimataifa juu ya udhibiti wa dawa za kulevya na kuiunganisha Mamlaka na jumuiya za kitaifa, kikanda na kimataifa zinazojishughulisha na mambo yanayohusiana na udhibiti wa dawa za kulevya.

Taasisi za usimamizi wa Mazingira ni miongoni mwa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ambazo zinajumuisha Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (ZEMA) na Idara ya Mazingira.

Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (ZEMA) imeanzishwa mwaka 2015 chini ya kifungu cha 14 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namb. 3 ya mwaka 2015. Lengo Kuu la Mamlaka hii ni kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria, kanuni, miongozo na viwango vya mazingira kwa ajili ya kupunguza uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Mamlaka ni Wakala wa Serikali wa masuala ya Mazingira.

Kazi za Mamalaka ya Mazingira ni kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Mazingira; kuratibu hatua za tathmini za athari za kimazingira; kuratibu ukaguzi wa kimazingira; kufanya ufuatiliaji wa kimazingira; kutoa vyeti, ruhusa au uthibitisho wa kimazingira; kupokea na kuyafanyia kazi malalamiko yanayohusiana na mazingira; kuendeleza elimu ya mazingira, ufahamu, na usambazaji wa taarifa kwa jamii na wadau wengine; kufuatilia bioanuwai, mifumo ya ikolojia; pamoja na kuandaa usalama na ulinzi wa kimazingira.

Idara ya Mazingira ni Taasisi nyingine ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais yenye jukumu la kuhakikisha kuwa nyenzo za usimamizi wa mazingira zinakuwepo; kutoa elimu ya mazingira kwa jamii pamoja na kuratibu masuala ya mabadiliko ya tabianchi.

Kazi za Idara ya Mazingira ni kutayarisha mikakati na miongozo ya kitaifa ya usimamizi wa mazingira; kutayarisha na kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Tathmini ya Kimazingira; kupendekeza viwango vya kimazingira; kuratibu utekelezaji wa mikataba ya kimataifa ya kimazingira; kuandaa na kutoa ripoti ya hali halisi ya kimazingira; kuratibu masuala ya mabadiliko ya tabianchi pamoja na shughuli za kuhimili na kukabiliana na athari za mabadiliko hayo; kuratibu na kuendeleza utafiti wa kimazingira; na kutekeleza kazi nyengine yoyote katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake.

# Kampeni ya kijana kataa UKIMWI Zanzibar

"Kijana Kataa UKIMWI" ni kampeni inayowalenga vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24 kwa lengo la kuwapatia elimu ya VVU na UKIMWI kwa kutumia mbinu bunifu zitakazowavutia na kuwahamasisha kushiriki kupata elimu ya UKIMWI na hatimae kubadilisha tabia. Kampeni ya Kijana kataa UKIMWI imekuja baada ya kuonekana kuwa vijana wengi ndio wahanga wa maambukizo mapya ya Virusi Vya UKIMWI katika ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara ikiwemo Zanzibar.

Aidha, vijana wamekuwa wakijihusisha sana na tabia hatarishi kama vile za utumiaji wa vilevi, kushiriki katika ngono zembe, kuwa na wapenzi wengi kwa wakati mmoja, mimba za utotoni na kujiingiza katika tabia ya kufanya ngono mapema, ambazo zote huwaweka katika hatari ya kupata maambukizo ya VVU wakiwa bado vijana wadogo.

Hapa Zanzibar inakisiwa kuwa hadi kufika Machi 2021, kati ya watu 7,598 wanaoishi na VVU, kati yao 632 ni vijana. Changamoto ya maambukizo mapya ya VVU kwa vijana imewakuta wengi wao wakiwa na uelewa mdogo na ukosefu wa ufahamu sahihi wa masuala ya VVU na UKIMWI. Utafiti wa Viashiria na Matokeo UKIMWI Tanzania (THIS 2016/17) ulionesha kuwa asilimia 24.6 tu ya vijana wenye umri katika ya miaka 15 hadi 24 ndio wenye uwelewa sahihi wa kujikinga na maambukizi ya VVU hapa Zanzibar.

Kwa mantiki hiyo, Tume ya UKIMWI kwa kushirikiana na Shirika la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) imekuwa ikitekeleza kampeni hii tangu 2017 hadi leo kwa lengo la kuwafikishia elimu vijana wengi kupitia mbinu bunifu zenye mvuto ikiwemo michezo mbali mbali.



*Upimaji wa VVU kwa vijana wakati wa bonanza*



*Mshiriki katika kampeni ya Kijana kataa UKIMWI akifukuza Kuku katika mchezo huo katika bonanza lililofanyika Wilaya ya Kaskazini A*

Kwa mwaka wa 2020 shughuli mbali mbali zilifanyika katika kampeni hii kama vile Chemsha bongo zinazohusiana na elimu ya VVU na Afya ya uzazi kwa wanafunzi wa skuli za Mkoa wa Mjini Magharibi, bonanza la mpira wa miguu, uchoraji wa ujumbe wa UKIMWI na Afya ya uzazi kwa baadhi ya skuli za msingi Unguja na Pemba.

Tume ya UKIMWI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iliratibu na kuendesha mashindano ya chemsha bongo yaliyofanyika katika ukumbi wa skuli ya John Pombe Magufuli na kuhusisha skuli sita za sekondari ambazo ni; Skuli ya John Pombe Magufuli, Skuli ya SUZA, Skuli ya Lumumba, Skuli ya High View, Skuli ya Glorious Academy na Skuli ya Biashara.

Mashindano yalizinduliwa na Mkurugenzi wa Elimu ya Sekondari, Bi Asya Iddi ambae katika hotuba yake aliwataka wanafunzi kutojihusisha kabisa katika vitendo viovu kama kutumia dawa za kulevya, ulawiti na ngono; badala yake washughulikie masomo yao ili waweze kutimiza ndoto zao.

Tume ya UKIMWI ilifanya mashindano ya chemsha bongo yaliyohusisha kuchagua na kujibu masuali ya VVU kwa wanafunzi wa skuli za Sekondari. Masuali mbali mbali yanayohusiana na elimu, mitazamo na matendo juu ya VVU na Afya ya Uzazi yaliulizwa kwa wanafunzi hao. Lengo lilikuwa ni kuwaweka vijana katika uwelewa sahihi wa masuala ya UKIMWI na Afya ya uzazi. Mshindi wa mashindano ya chemsha bongo ilikuwa ni skuli ya Sekondari SUZA ikifuatiwa na Lumumba.

Aidha, Tume ya UKIMWI kupitia kampeni ya kijana kataa UKIMWI ilifanya bonanza la mpira wa miguu ili kuwafikia vijana wa kiume na kuwapa elimu ya VVU na huduma za upimaji.

Bonaza la mpira wa miguu lilifunguliwa na aliyekuwa Katibu Mkuu katika Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo Bw. Omar Hassan Kingi kwa kuwaasa vijana kutojihusisha na tabia hatarishi ambazo zinaweza kuwapelekea kupata maambukizo ya VVU na UKIMWI.

Timu zilizopambana ni Machicha FC kutoka Nyerere na Prince FC kutoka

*Inaendelea Uk. 9...*

# Kampeni ya kijana kataa UKIMWI Zanzibar



***Aliekuwa Katibu Mkuu Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo Bw. Omar Hassan Kingi akikagua timu zilizocheza bonanza la mpira wa miguu.***

***Inatoka Uk. 8***

Daraja bovu. Mshindi wa bonanza hiyo alikuwa ni timu ya Machicha FC na kujinyakulia fedha taslim shilingi laki tano (500,000) na mipira miwili na timu ya Prince FC ilipata ushindi wa pili na kuzawadiwa fedha taslim shilingi laki mbili na elfu hamsini (250,000) na mpira mmoja.

Kampeni ya kijana kataa UKIMWI pia iliwafikia wanafunzi wa Skuli 36 za msingi na maandalizi, Unguja 24 na Pemba 12, na kuwapatia elimu kwa njia mbali mbali ikiwemo michoro inayohusiana na VVU, Afya ya uzazi, kupinga unyanyapaa, utumiaji wa ARV, kupinga ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwenye kuta za skuli zao. Lengo ni kuwajengea uwezo watoto kukabiliana na changamoto mbali mbali zinazokwamisha mustakabali wa maisha yao na kuchochea maambukizi ya VVU na UKIMWI. Skuli zilizoshiriki ni Skuli za msingi Regeza Mwendo, Mbuzini, Bububu na Kianga kwa Magharib A; Skuli za msingi Kinuni, Kiembe Samaki na Mwanakwerekwe kwa Wilaya ya Magharib B.

Aidha, Skuli za Msingi za Muungano, Darajani na Mwembe Makumbi kwa Wilaya ya Mjini; Skuli za msingi Nungwi, Mkokotoni, Matemwe na Kinyasini kwa Wilaya ya Kaskazini A; Skuli za msingi Mahonda, Mgonjoni, Fujoni, Mgambo na Kitope kwa Wilaya ya Kaskazini B; Skuli za Mrembo, Safia Rijali, Jendele, Ng'ambwa na skuli ya maandalizi ya Mpapa kwa Wilaya ya Kati zilishiriki.

Kwa upande wa Wilaya ya Wete Skuli zilizoshiriki ni Minungwini, Mzambarauni na Kizimbani. Skuli za Ngwachani, Ng'ombeni na Mwambe kwa Wilaya ya Mkoani; Skuli za Ziwani, Michakaini na Vitongoji kwa Wilaya ya Chake Chake na Skuli za Makangale, Konde na Micheweni kwa Wilaya ya Micheweni nazo pia zilishiriki.

Hakuna Wilaya iliyoachwa nyuma katika kampeni ya Kijana kataa UKIMWI. Vijana wengi wa kike kwa kiume wa Unguja na Pemba walifikiwa na Kampeni hii kwa elimu ya VVU na Afya ya uzazi ikiwa ni pamoja na huduma za ushauri nasaha na upimaji wa hiari wa VVU.

Kila wilaya iliendesha shughuli mbali mbali za kuwahamasisha vijana kujitokeza kwa wingi katika huduma kama vile mpira wa miguu, nage, kufukuza kuku, sarakasi, kuvuta kamba, kukuna nazi, kunywa maji, kula maandazi na kujaza maji. Aidha, kulifanyika kongamano la vijana kwa wanafunzi wa skuli za sekondari na vyuo vikuu, upimaji wa VVU na ugawaji wa vipeperushi.

Kufuatia shughuli zote zilizofanyika katika kampeni ya kijana kataa UKIMWI, huduma ya ushauri nasaha na upimaji wa VVU ilichukuwa nafasi kubwa ambapo jumla ya vijana 4,628 walifikiwa kwa elimu na vijana 3,098 walipima VVU. Katika upimaji huo kijana mmoja aligundulika na maambukizi ya VVU na kupelekwa katika kituo cha huduma na tiba ya UKIMWI.




***Wanafunzi wa skuli zilizoshiriki katika mashindano ya chemsha bongo katika ukumbi wa skuli ya John Pombe Magufuli.***

# Mhe. Othman ahimiza juhudi za pamoja kurejesha Z'bar ya kijani

## ● Akumbusha Wazanzibari kufahamu miti ni uchumi
## ● Ashauri jamii kupunguza matumizi ya mkaa



***Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Othman Masoud Othman akipanda mti katika makaazi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Micheweni Pemba ikiwa ni shamra shamra za kuelekea maadhimisho ya Siku ya Mazingira 2022 yaliyoadhimishwa kitaifa katika viwanja vya Mnazimmoja Wete Pemba.***

"Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, pamoja na mambo mengine mtambuka, inajukumu la kusimamia hifadhi ya Mazingira ya Zanzibar.

Katika kutekeleza jukumu hilo imeandaa mpango mkubwa wa kupanda miti ya aina mbali mbali Unguja na Pemba ili kuhakikisha kwamba Zanzibar inarudi katika uasili wake wa kijani".

Hii ni kauli ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Mhe. Othman Masoud Othman, aliyoitoa kwa nyakati tofauti Unguja na Pemba akiwa katika ziara zake za kukagua na kuona hali halisi ya mazingira na kuhimiza jamii ya Wazanzibari kuungana na viongozi kwa pamoja ili kujenga tabia na utamaduni wa kushiriki kupanda miti.

Mhe. Othman amesema kwamba, miti licha ya kuwa muhimu sana katika kusaidia kuhifadhi mazingira, pia ina faida kubwa kiuchumi na inaweza kusaidia kuinua kipato kwa wananchi iwapo watatilia maanani suala hilo kibiashara na kiuchumi.

Katika maelezo yake ya kuwahamasisha wananchi kupanda miti, Mhe. Othman ametoa mfano kwamba mti mmoja wa mtondoo unaweza kuuzwa kwa wastani wa hadi shilingi laki tatu za Tanzania na iwapo mwananchi atakuwa amefanya juhudi ya kupanda angalau miti 3,000 atakuwa na uwezo wa kupata kiasi cha shilingi milioni 900, fedha ambazo ni nyingi na hakuna kazi inayoweza kuzalisha kiwango cha fedha kama hicho kwa wepesi kwa mwananchi wa kawaida.

Mhe. Othman amefahamisha kwamba, mbali na hatua hiyo, pia Wananchi wanapofanya juhudi za kuunga mkono Serikali na viongozi kupanda miti ya chakula, kivuli, biashara na matunda pia ni njia muhimu ya kuweza kukabiliana vyema na mabadiliko ya tabianchi na kulinda mazingira.

Amesema, Zanzibar kama zilivyo nchi nyingi duniani nayo inakumbwa na athari kadhaa zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi ambapo juhudi za pamoja kupitia mikakati, sera na sheria ni njia muhimu na muafaka za kukabiliana na hali hiyo.

Amesema kwamba ongezeko la joto duniani linachangia kuyayuka kwa barafu katika vilele vya milima na hivyo kuongeza kina cha maji baharini na kwamba fukwe nyingi za Unguja na Pemba zimekumbwa na uharibifu mkubwa wa mazingira kwa kuwa na mmong'onyoko huku maji ya chumvi yakiendelea kula ardhi iliyo karibu na bahari.

Takwimu za kiutafiti zinaonesha kwamba maeneo mengi ya fukwe kama vile Nungwi, Jambiani, Vumawimbi na kwengineko tayari zinahitajika jitihada kubwa za kuhifadhiwa kwa kuwa mabadiliko hayo ya tabianchi yamesababisha mmong'onyoko mkubwa wa fukwe za asili na maji ya chumvi kusogea na kutafuna ardhi ambayo husababisha pia wananchi kupungukiwa na maeneo ya kilimo.

Aidha Mhe. Makamu amesema kwamba jitihada hizo ni muhimu kuendelezwa na kuungwa mkono na watu wote kwa kuwa ni hatua muhimu itakayosaidia kuifanya Zanzibar kuwa ya kijani kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Mhe. Othman amewakumbusha wananchi kwamba jukumu hilo la kulinda na kuhifadhi mazingira ni lazima litekelezwe na kila mmoja miongoni mwa wanajamii, viongozi na wanajumuiya ambao kwa pamoja wanapaswa kujenga tabia ya kupanda miti hata pembezoni mwa makaazi yao wanayoishi.

Amesema Serikali inaendelea na juhudi

***Inaendelea Uk. 11...***

# Mhe. Othman ahimiza juhudi za pamoja kurejesha Z'bar ya kijani

*Inatoka Uk. 10*

za kulinda na kuhifadhi mazingira na kuweka mipango, sera, sheria na mikakati madhubuti mbali mbali itakayosaidia kuifanya Zanzibar kuwa ya kijani na kuwataka wananchi wote kujitahidi kuunga mkono jitihada hizo ambazo ni muhimu kwa maisha ya wanaadamu na viumbe wengine duniani.

Amewataka wanajamii kuacha tabia ya kuyafanya maeneo ya pori kuwa majangwa kwa kukata miti ovyo na badala yake wafanye jitihada kuyageuza maeneo ya majangwa kuwa mapori ili kusaidia vyema hifadhi ya mazingira.

"Haya ni mambo yanayowezekana, wenzetu walikuwa na majangwa makubwa kwa jitihada wamefanikiwa kuyageuza mapori, lakini sisi tuna mapori tunayageuza majangwa, pengine tunakata miti kwa ujenzi wa nyumba hata mahali pasipostahiki. Jambo hili ni lazima kulikataa", alisisitiza Mhe. Makamu.

Mhe. Othman amewakumbusha wananchi kufahamu kwamba kama walivyo wengine wengi duniani, nao hawawezi kuishi bila ya kuwepo miti na kuonya kwamba wasiendeleze tabia ya kuyageuza mapori kuwa majangwa kwa kukata miti ovyo jambo ambalo linaathari kubwa kwa nchi na jamii kwa jumla.

Akizungumzia uharibifu wa mazingira katika uchimbaji wa mawe na mchanga katika maeneo yasio rasmi, Mhe. Othman amezitaka mamlaka za Wilaya na Mikoa kuhakikisha wanashirikiana na Vyombo mbali mbali ili kutenga maeneo na kuyarasimisha kwa ajili ya upatikanaji wa rasilimali hiyo jambo litakalopunguza uchukuaji na utumiaji kiholela wa rasilimali hiyo.

Tafiti zinaonesha maeneo kama vile Fumba, Vitongoji, Micheweni, Kwareni Pujini na sehemu kadhaa ni miongoni mwa maeneo yaliyoharibiwa sana kwa uchimbaji wa mawe na kokoto kiholela.

Katika ziara yake kwenye maeneo hayo Mhe. Makamu aliziagiza Mamlaka kuhakikisha kwamba wanapokuwa na miradi ya maendeleo wanaingiza pia gharama za kurejesha hali ya asili kwa maeneo yaliyochukuliwa rasilimali kama vile mchanga na mawe ambayo imetumika



***Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Harusi Said Suleiman akipanda mti aina ya mpera huko katika makaazi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Micheweni Pemba ikiwa ni shamra shamra za kuelekea maadhimisho ya Siku ya Mazingira 2022 yaliyoadhimishwa kitaifa katika viwanja vya Mnazimmoja Wete Pemba.***

katika miradi hiyo ya maendeleo.

Amesema miradi ya maendeleo, lazima iwe na uwiano na mazingatio makubwa katika suala la hifadhi ya mazingira ili kuendelea kuilinda Zanzibar na uharibifu mkubwa wa mazingira kwenye maeneo yote.

Kwa upande mwengine Mhe. Makamu wa Rais ameitaka jamii kuendeleza mashirikiano na vyombo mbali mbali vya Serikali na binafsi katika kuhakikisha kwamba suala la upandaji miti linapata msukumo stahiki ili dhamira ya kuhakikisha Zanzibar inakuwa ya kijani iweze kufanikiwa.

Mhe. Othman amesema kufanikiwa kwa mpango huo wa Serikali, kunahitaji ushiriki wa kila mtu miongoni mwa wanajamii ikiwa ni pamoja na wananchi kujenga na kuendeleza utamaduni wa kudumu wa kuhakikisha kila mmoja anapanda miti ikiwemo maeneo ya pembezoni mwa nyumba za kuishi.

Aidha amewakumbusha viongozi wa mikoa na wilaya kuhakikisha kwamba wanasimamia vyema suala la Mipango miji ili kuondosha ujenzi holela unaofanywa katika maeneo mbali mbali.


Kwa Upande Mwengine Mhe. Makamu wa Rais amewakumbusha wananchi kupunguza matumizi ya mkaa kwa kuwa matumizi ya nishati hiyo ni chanzo kikubwa cha ukataji miti ovyo jambo ambalo linachangia sana uharibifu wa mazingira nchini.

Sambamba na hilo Mhe. Othman, amewataka wananchi kuhakikisha waendeleza usafi katika maeneo yote nchini ikiwa ni pamoja na mmalaka husika kusimamia kwa makini suala la utupaji wa taka ambalo ni chanzo kikubwa cha kuchafua mazingira.

Amesema ni vyema wananchi kuziona na kuzigeuza taka kwamba ni bidhaa muhimu inayoweza kuwasaidia kupata fursa ya kipato badala ya kuwa uchafu na wanapaswa kuziweka katika mahala stahiki ambapo zinaweza kutumika kwa uzalishaji katika kazi za kilimo.

Mhe. Othman amesema serikali inafanya jitihada na kutumia gharama kubwa ya fedha na nguvu za wananchi ili kuhakikisha kwamba maji ya chumvi hayaendelei kuathiri jitihada za wakulima wa mpunga katika mabonde mbali Unguja na Pemba.

## IJUE LUGHA YA ALAMA KWA VIZIWI




## Utambulisho wa maneno na matumizi sahihi ya lugha kwa Watu wenye Ulemavu

1) Sio sahihi kumuita Taahira, Halfani, chizi, ........Jina sahihi ni Mtu mwenye Ulemavu wa Akili

2) Sio sahihi kumuita Mzungu, zeruzeru, dili,...... Jina sahihi ni Mtu mwenye Ulemavu wa Ualbino

3) Sio sahihi kumuita Bubu..... Jina sahihi ni Mtu mwenye Ulemavu wa Uziwi

4) Sio sahihi kumuita Kiwete, Dosti Jina sahihi ni Mtu mwenye Ulemavu wa Viungo

5) Sio sahihi kumuita Kipofu Jina sahihi ni Mtu mwenye Ulemavu wa Uoni

6) Sio sahihi kumuita mbilikimo ......Jina sahihi Mtu mwenye Ulemavu wa kudumaa



***Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Dkt Omar D. Shajak, ameiongoza Kamati ya Kudumu ya Viwanda, Biashara na Mazingira ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetembelea Mradi wa EBBAR ikiwa ni ziara ya kutembelea maeneo ya mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabia nchi kwa kutumia ekolojia (EBBAR) unaosimamiwa na Ofisi ya Makamo wa Rais Muungano na Mazingira kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Zanzibar Wilaya ya Kaskazini "A" katika Shehia za Matemwe Kijini, Mbuyutende, na Jukakuu Wadi wa Kijini.***



***Kikao cha mashauriano ya pamoja kati ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu na Ujumbe kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu wenye lengo la kukuza ushirikiano na kubadilishana uzoefu hasa katika sekta ya Watu wenye Ulemavu kilichofanyika ukumbi wa mkutano Migombani.***




***Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar Dkt Omar D. Shajak akimkabidhi Bw Ali Omar Ali, Jokofu kufuatia utumishi uliotukuka kwa kusimamia vyema kazi za ulinzi katika taasisi tofauti hadi anastaafu kwenye Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Zanzibar***



***Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Harusi Said Suleiman na watendaji wakuu wa ofisi hiyo wakiwa na Kamati ya kusimamia ofisi za viongozi wakuu wa kitaifa ya Baraza la Wawakilishi kwa pamoja na Jumuiya ya Uhifadhi wa Mazingira ya Chaani Kikobwe ni walipotembelea kitalu cha miche ya matunda na baadaye kushiriki zoezi la upandaji ili kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Jumuiya hiyo.***

# Jamii ijiepushe na udhalilishaji kwa Watu wenye Ulemavu



*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Dkt Omar D.Shajak akimkabidhi kiti cha magurudumu mawili chenye kutumia chaji ( Motor Wheel Chair) Bi Zahra Wazir Said kutoka skuli ya sayansi na Tiba Mbweni Chuo Kikuu cha SUZA anaechukuwa Stashahada ya Famasia.*

Ni vyema ikaeleweka kwamba, Watu wenye Ulemavu, hasa wale wanaoishi katika mazingira magumu, wana asilimia kubwa ya kuweza kudhalilishwa ikilinganishwa na wale wasiokuwa na ulemavu.

Udhalilishaji mara nyingi hufanywa na mtu aliyezoeleka na mtu anayefanyiwa udhalilishaji. Mtu huyu anayeaminika anaweza kuwa yumo miongoni mwa familia moja, wafanyakazi wanaosaidiana, mwenzake wa karibu, wa rika moja na inawezekana ikawa wanaishi pamoja.

Sheria ya Watu wenye Ulemavu (Haki na Fursa) Namb. 9 ya mwaka 2006 na Sheria ya Mtoto Namb. 6 ya mwaka 2011 ni Sheria zinazowalinda watu hawa dhidi ya vitendo vya udhalilishaji ambapo inatoa uhifadhi kwa Watu wenye Ulemavu na hivyo hupatiwa huduma za matunzo.

Ingawaje, katika Sheria hizo uhifadhi wa moja kwa moja haupatikani kwa Watu wenye Ulemavu.

Makala hii inakusudia kuwajengea uwezo wasomaji wake waweze kujiamini, kuyajua mazingira ya Watu wenye Ulemavu, namna walivyo na jinsi ya kuweza kuwasaidia katika maeneo mbalimbali kama vile katika maeneo ya kazi, sehemu za ibada na katika jamii.

Udhalilishaji unaweza kugawika katika aina tofauti. Aina hizo ni Udhalilishaji wa kimwili, Udhalilishaji wa Kingono, Udhalilishaji wa bila ya ridhaa ya mwenyewe na udhalilishaji kihisia.

Udhalilishaji wa kimwili ni wa dhahiri na ni maarufu. Katika aina hii ya udhalilishaji muhusika hupata madhara ya kiwiliwili kama vile yanayotokana na kupigwa, kuvutwa nywele, kupigwa mateke na kutikiswa bila kiasi; kuunguzwa moto kama vile pasi na sigara; kuongozwa visivyo sahihi; na kufunzwa visivyo sahihi kutegemea na silka, mila na desturi. Mfano wa haya ni kama vile kula, kujisaidia, na mambo mengine yanayofanana na haya.

Ishara za kudhalilishwa kimwili ni kama michubuko, kumuogopa mtu maalum, kutokumuamini mtu, kufanyiwa vitendo au kuingizwa kitu kikakupelekea kupata uwasho na kuwa na wasi wasi wakati wote kwa mtu maalum.

Kuna njia kadhaa zinazoweza kutumika kuepuka kudhalilishwa kimwili. Njia hizo zinajumuisha kuinua uelewa wa Watu wenye Ulemavu kuhusu aina tofauti za udhalilishaji na haki za binadamu kwa njia ambazo ni rahisi kueleweka kwa Watu wenye Ulemavu. Mfano wa njia hizo ni kutumia lugha ya alama.

Njia nyengine zinazoweza kutumika ni kubadilisha mitazamo juu ya Watu wenye Ulemavu kutoka mtazamo hasi kwenda mtazamo chanya, kubadilisha sera na sheria ili ziendane na kuepuka udhalilishaji kwa Watu wenye Ulemavu, kukuza uelewa kwa jamii juu ya Watu

*Inaendelea Uk. 15...*

# Jamii ijiepushe na udhalilishaji kwa Watu wenye Ulemavu



***Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Harusi Said Suleiman akiwa na wajasiriamali kutoka kituo cha mafunzo ya mapishi kwa Watu wenye Ulemavu kilichopo Tomondo.***

***Inatoka Uk. 14***

wenye Ulemavu, haki na fursa zinazowahusu na kutoa elimu kwa jamii ya mahitaji ya Watu wenye Ulemavu wanaofanyakazi nao.

Udhalilishaji wa kingono unapatikana pale ambapo mtu mwenye ulemavu anafanyiwa udhalilishaji bila ya kumjuilisha na kukosa ridhaa yake. Udhalilishaji wa bila ya ridhaa ya mwenyewe unajumuisha kukaribisha vitendo, maoni maneno au kukaribisha tabia za udhalilishaji; kumgusa mtu makalio au sehemu za siri; kuonesha video au picha za ngono; kumuonesha mtu mwenye ulemavu katika video kwa vitendo vya uharamia, na mambo mengine yanayofanana na hayo.

Dalili za udhalilishaji wa kingono unajumuisha kujisaidia mbele yake bila ya kujihifadhi, kumuambukiza maradhi ya kujamiiana, kusitasita wakati wa kuongea na kukataa kuhudhuria maeneo ya kawaida.

Udhalilishaji Kihisia ni aina nyengine udhalilishaji. Huu hujumuisha uonevu, kejeli za maneno, kumtia unyonge, kumfanyia vitisho, kumuondoshea kisaidizi kama vile kiti cha magurudumu na kumtoa kisaidizi chakusikilizia.

Dalili za udhalilishaji kihisia zinajumuisha uchokozi, kumdhuru mwenyewe, mabadiliko ya hisia yasiyoelezeka, kutokumthamini au kumthamini kwa kiwango cha chini, na kumsababishia huzuni.

Iwapo kila mmoja kwa nafasi yake, atachukua hatua stahiki bila shaka udhalilishaji wa aina zilizotajwa hapo juu utapungua au kuondoka kabisa. Hivyo jitihada za makusudi zinapaswa kuchukuliwa katika kutoa elimu ya masuala ya Watu Wenye Ulemavu ili kuepuka udhalilishaji katika jamii yetu.

# Zijue dawa za kulevya na madhara yake







**Na Arafa Hussein**

BILA shaka utakubaliana nami kwamba katika hali ya kawaida wengi wamezoea kusikia msamiati maarufu wa dawa za kulevya.

Ufahamu wa dhana hii miongoni mwa wanajamii sio sawa.Wapo wenye uelewa kwa kiwango kidogo, wengine cha kati na baadhi hawafahamu bali wanasikia tu neno hilo. Hata hivyo, watakuwepo wenye uelewa zaidi hasa kwa vile wapo wanaotumia muda mwingi kushughulikia mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Makala hii inalenga kufafanua kiundani juu ya dhana hii ya dawa za kulevya hasa katika kipengele cha madhara yatokanayo na matumizi ya dawa hizo. Dawa za kulevya sio msamiati mgeni miongoni mwa watu wote hivi sasa na unafahamika sana.

Wataalamu mbalimbali katika kada za Saikolojia, Biolojia na hata Wanaharakati wa shughuli za kijamii duniani kote wamenukuliwa kwenye machapisho yao tofauti wakitoa maana ya dawa za kulevya kwamba ni chochote au kemikali ambazo mtu akizitumia huathiri mfumo wa fahamu na kuleta mabadiliko katika hisia, fikra na tabia hatua kwa hatua.

Kwa mnasaba wa tafsiri hii utakubali kuwa vitu au kemikali hizi zimetapakaa katika jamii. Wataalamu hao wameainisha makundi makuu manne ya dawa za Kulevya kulingana na jinsi zinavyoathiri mfumo wa ufahamu wa mtumiaji.

Kundi la kwanza ni Vichangamshi (Stimulants), la pili Vikandamizi (Depressants) la tatu ni Vileta njozi (Hallucinogens) na la mwisho ni Kasumba (opium).

Vichangamshi: Inadaiwa kuwa mtumiaji wa dawa hizi humpelekea kuchangamka. Mfano wa dawa hizo ni kokeini (unga), mirungi, bangi, amphetamine, tumbaku na mazao yake (sigara, kuber) na caffeine.

Vikandamizi: Hizi inaaminika zinakandamiza ufanyaji kazi wa ubongo, kuleta usingizi na kudorora mwili. Mfano wa dawa hizo ni gongo, konyagi, whisky, mataputapu, na dawa za kuleta usingizi (kama valium, phenobarbitone na mandrax).

Vileta njozi: Hizi hutoa mapokezi na hisia tofauti kwa mtumiaji na husababisha mtumiaji kuhisi, kuona au kusikia vitu visivyokuwepo au tofauti na uhalisia. Mfano wa dawa hizi ni lysergic acid diethylamide, Ecstasy (Molly/ molecular), Mescaline & Peyote (cactus).

Kasumba: Inadaiwa kwamba dawa hizi huondoa maumivu makali, zinaleta utulivu na inaaminika kwamba zinaleta raha. Mfano ni Heroin (unga), Pethedine, Morphine, Methadone na Codeine.

Aina zote za dawa hizi inaaminika zinapatikana na zinatumiwa na vijana mbali mbali Zanzibar, ingawa nyingi ya hizo hazizalishwi hapa zanzibar.

Tafiti zinaonesha kuwa dawa za kulevya Zanzibar zinapatikana kupitia vyanzo mbali mbali ikiwemo uingizwaji kutoka nje. Dawa hizi ni kama vile Heroin, Cocaine na Metamphetamine. Pia zinapatikana kwa kuwepo uchepushwaji wa dawa tiba zenye asili ya kulevya na utengenezaji katika maabara haramu kwa kutumia kemikali bashirifu.

Licha ya kuwa dawa za kulevya hazina faida yoyote kwa mtumiaji, bado kuna kundi kubwa la watu, hasa vijana, wanaendelea kutumia dawa hizi na kila siku wanaongezeka.

Tafiti mbali mbali za kitaalamu juu ya janga hili zinaonesha kuwa watumiaji wengi wa dawa za kulevya wamejiingiza kwenye matumizi kutokana na sababu tofauti ikiwemo shindikizo rika, migogoro ya familia, kukosa malezi bora, uelewa mdogo wa stadi za maisha, ukosefu wa kazi, kutokujua madhara, upatikanaji rahisi wa dawa hizo, ugumu wa maisha, utandawazi na imani potofu kwa kazi ngumu kama za uvuvi, ujenzi, kubeba mizigo au ukahaba.

Kijana aliyeathirika kwa moja ya sababu hizo au zote kwa pamoja, kuna uwezekano mkubwa wa kutumbukia katika kundi haramu la watumiaji wa dawa za kulevya.

*Inaendelea Uk. 17...*

# Zijue dawa za kulevya na madhara yake

*Inatoka Uk. 16*

Katika hatua hizi unaweza kumgundua kijana anayeanza kutumia dawa za kulevya kwa kuangalia dalili au tabia anazoibuka nazo kama vile kuwepo mabadiliko ya tabia, kujihusisha na marafiki wapya ambao hawaendani naye, kujitenga na kuwa msiri, kubadilika na kuwa mkali na mwenye hasira, kubadilika ghafla kwa malengo yake, kubadilika muonekano wake (uchafu, sura), kuwa na tabia ya udokozi, kuuza vitu vyake, madeni mengi na kukosa hamu ya kula.

Tabia ya utumiaji wa dawa za kulevya ikiendelea na kuzoeleka ndani ya mwili, mtumiaji anageuka kuwa 'mteja' wa dawa za kulevya. 'Uteja' ni ugonjwa sugu unaotokana na matumizi ya dawa za kulevya na huathiri ubongo hasa upande wa fikra, hisia na tabia.

Hali hii humfanya mtumiaji kuona kwamba dawa za kulevya kwake ni mahitaji ya lazima pamoja na kufahamu madhara yatokanayo na matumizi ya dawa hizo.

Hali hii hutokea kwa sababu mtu akitumia dawa za kulevya, huingia kwenye damu na huenda kwenye sehemu ya ubongo iitwayo limbic system. Sehemu hii inahusika na kuleta raha.

Dawa za kulevya zikifika kwenye ubongo husababisha kutolewa kwa wingi kemikali iitwayo Dopamin ambayo inahusika na kuleta raha. Mtumiaji inadaiwa hupata raha isiyo kifani, hivyo kumfanya mtu kuendelea kutumia dawa za kulevya. Kwa kadri mtumiaji anavyotumia huongeza kiwango .

Matumizi ya dawa za kulevya kwa muda mrefu husababisha athari kadhaa katika mwili wa binaadamu ikiwemo ubongo na husababisha kupoteza uwezo wa kufikiri, uwezo wa kufanya maamuzi, kutoweza kujifunza, kukosa uwezo wa kutunza kumbukumbu na akili kuvurugika.

Wataalamu wa masuala haya wanabainisha kuwa hakuna utafiti wowote duniani ulioonesha kuwa dawa za kulevya zina faida katika mwili wa binadamu.

Aidha wataalamu hao wanasema kuwa hakuna chembe ya faida endelevu ya dawa za kulevya kwa binadamu, bali husababisha majanga kiafya, kiuchumi, kijamii, kidiplomasia, kimazingira na kiusalama. Madhara mengine kwa mtumiaji ni kuwepo uwezekano wa maambukizi ya virusi vya UKIMWI, homa ya ini B na C, magonjwa ya mapafu, akili, magonjwa ya ngozi, magonjwa ya kinywa na hata vifo vya ghafla.



***Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Harusi Said Suleiman akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa kituo hicho Simai Maulid Amour alipofanya ziara katika kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Kidimni.***

Athari za dawa za kulevya kijamii husambaratisha familia, kuongezeka idadi ya mayatima, kuporomoka maadili, utoro skuli na mimba zisizotarajiwa.

Pia dawa za kulevya huathiri uwezo wa mtumiaji kufanya kazi, na pia rasilimali za Taifa hutumika kuwatibu waathirika na kudhibiti wafanyabiashara wa dawa za kulevya.

Madhara ya kiuchumi yatokanayo na dawa za kulevya ni pamoja na kuvuruga uchumi wa nchi kwa njia mbali mbali zikiwemo mzunguko haramu wa fedha kunakochangia mfumko wa bei, kuhodhiwa kwa uchumi na wachache na kuwepo kwa uwekezaji haramu.

Kimazingira, athari za dawa za kulevya ni kusababisha uchafu kutokana na utupaji ovyo wa bomba za sindano, kuhatarisha usalama kwa wapita njia na kusambaza vijidudu vinavyoeneza maradhi.

Kiusalama matumizi ya dawa za kulevya yana athari kubwa kwa vile husababisha vita vya wenyewe kwa wenyewe, ugaidi, uharamia na mapinduzi ya tawala halali.

Katika kupunguza ongezeko la watumiaji wa dawa za kulevya na kupiga vita biashara ya dawa za kulevya, Serikali kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya imeanzisha mikakati kadhaa ya kuzuia biashara hiyo haramu. Katika kutekeleza majukumu yake hayo ya kupiga vita utumiaji na biashara ya dawa za kulevya, Mamlaka inaendesha operesheni za kuwagundua na kuwakamata wafanyabiashara wa dawa za kulevya na dawa zenyewe, kuteketeza dawa za kulevya, kudhibiti uchepushaji wa kemikali bashirifu, kudhibiti uchepushaji wa dawa tiba zenye asili ya kulevya pamoja na ufuatiliaji wa kesi za dawa za kulevya.

Licha ya juhudi hizo, mapambano dhidi ya dawa za kulevya yanakabiliwa na changamoto nyingi. Miongoni mwa changamoto hizo ni uhaba wa rasilimali fedha na rasilimali watu, maumbile ya mipaka ya nchi ardhini na baharini, pamoja na uelewa mdogo miongoni mwa jamii juu ya madhara ya biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

# Kuzingatia haki za Wenye Ulemavu ni wajibu wetu sote



***Mkurugenzi BTWWU akiwasikiliza Madereva wa Bajaji Wenye Ulemavu ktk Bustani ya Jamhuri Garden na kuwapa Muongozo na maelekezo yatakayowasaidia ktk kuboresha utoaji huduma zao ili waweze kujikimu kimaisha***

**UKIZUNGUMZIA** haki za Watu wenye Ulemavu ni vyema ukaelewa maana ya ulemavu kimtazamo, kijamii na kisheria.

Maana ya ulemavu ni upungufu wa uwezo wa viungo vya mwili, akili au hisia unaomsababishia mtu kushindwa kumudu mazingira yake au kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii. Hii ni kwa mujibu wa tafsiri ya Sheria ya Watu wenye Ulemavu (Haki na Fursa) Namba tisa ya mwaka 2006.

Baadhi ya watu wanaamini kuwa, Watu wenye Ulemavu au kuwa na ulemavu ni sababu inayowakosesha baadhi ya haki zao zinazowahusu na hivyo kufanyiwa huruma au ukarimu ndio jambo wanalostahiki.

Makala hii itaangalia iwapo kuwapatia au kuwafanyia baadhi ya mambo Watu wenye Ulemavu ni miongoni mwa haki zao au ni ukarimu tu wa mtu husika kutokana na imani aliyonayo mtu huyo. Pia itaangalia athari za ulemavu na mtazamo wa jamii katika kuzingatia mambo yanayowahusu.

Ni vyema ikafahamika kwamba, haki sio huruma wala ukarimu. Huruma inaweza ikatolewa kwa ridhaa ya yule mtu anayetoa ukarimu lakini haki ni lazima itolewe kwa wanaostahiki kwani haki haina hiari.

Haki ni tabia au ulazima wa kisheria wa kufanya jambo lolote lile iwe kutoa au kupewa, kufanya au kufanyiwa sambamba na upatikanaji wa sheria ndogondogo kwa baadhi ya mifumo ya sheria za nchi husika.

Huruma ni kufanya jambo la msaada wa kihali kwa mtu katika mazingira yaliyomzunguka au mtu mwenye uwezo kutoa msaada wa kihali, kiuchumi au kifedha kwa mtu mwenye hali duni au anayehitaji msaada kwa wakati

***Inaendelea Uk. 9...***

# Kuzingatia haki za Wenye Ulemavu ni wajibu wetu sote

*Inatoka Uk. 8*

husika na kwa jamii husika.

Jamii zinatofautiana katika mitazamo juu ya Watu wenye Ulemavu. Kuna mitazamo mikuu miwili. Nayo ni mtazamo wa kiugonjwa na mtazamo wa masuala ya kijamii. Mitazamo hii ndio inayoonekana na walio wengi.

Mtazamo wa kiugonjwa ni njia moja wapo inayoangaliwa kwa Watu wenye Ulemavu. Kwa mujibu wa mtazamo huu, watu hawa wamewekwa katika mazingira maalum na jamii inayowazuguka. Hapa, kwa ufupi, ni masuala ya upungufu wa maumbile kibaiolojia ambayo yanachukuliwa kuwa ni matatizo yanayoweza kupelekea kupata ulemavu.

Kwa mujibu wa mtazamo wa kiugonjwa, kuyapatia ufumbuzi matatizo ya Watu wenye Ulemavu ni haki kukitengeneza kiwiliwili na akili na wakati mwingine huweza kupelekea gharama kwa watu wengine katika nyanja za maisha yao.

Kwa mujibu wa mtazamo huu, ni juu ya mtu mwenye ulemavu mwenyewe kuweza kabadilika katika kukabili mazingira yaliyomzunguka. Kwahiyo, ikiwa Watu wenye Ulemavu hawawezi kuyakabili na kuyatengeneza au kutengenezewa mazingira wanayoishi, watu hawa watakuwa kweli wana matatizo.

Mtazamo wa kiugonjwa unafanya ionekane kuwa kuna mambo ambayo Watu wenye Ulemavu hawawezi kuyafanya, wakati na hao watu wengine wasiokuwa na ulemavu pia yapo baadhi ya mambo hawawezi kuyafanya. Dhana hizi si sahihi na badala yake iwapo kutakuwa na uelewa mkubwa wa masuala ya Watu wenye Ulemavu ikiwemo haki zao na mahitaji yao dhana hizi na mitazamo hii iliyopo isingekuwepo kabisa.

Mtazamo wa jamii kwa Watu wenye Ulemavu ni kuwa sio hali ya ugonjwa au ukosefu wa kibaiolojia ambao unaweza kuibua ulemavu kwa wao wenyewe, lakini vikwazo vingi vinapatikana kihalisia, kisheria, mfumo wa kupata taarifa na mawasiliano pamoja na yale yote yanayohusu mtazamo, utamaduni na sababu mbalimbali katika jamii.

Ukweli ni kwamba, mtu mwenye ulemavu ni tofauti au anakuwa na mapungufu lakini mapungufu hayo hayawezi kumzuia mtu huyo kushiriki katika baadhi ya shughuli za kijamii.

Mara nyingi, mtazamo huu unatia hofu na una upungufu wa ufahamu wa mambo au utofauti wa ufahamu. Hivyo kuna haja ya mabadiliko ya hali ya juu ili kuibadilisha jamii tunayoishi kwa kuwapatia fursa mbali mbali na za kiwango bora cha maisha watu wote bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

Hivyo, mfumo huu wa kijamii unaeleza namna unavyopunguza mtazamo au athari hasi zilizoibuliwa na jamii yenyewe kwa kuwawekea vikwazo Watu wenye Ulemavu na kuzingatia umuhimu wa kutoa huduma zilizo na kiwango bora katika maisha.

Haki za Watu wenye Ulemavu tunaweza tukaziangalia katika maeneo matatu makuu nayo ni Haki za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

Kitaifa haki hizi zimeelezwa kwenye Katiba ya Zanzibar ya 1984, na ile ya Jamhuri ya Muungano ya 1977, Sera ya Watu wenye Ulemavu na Sheria ya Watu wenye Ulemavu 9 ya mwaka 2006. Haki hizo ni Haki ya matunzo, Haki na fursa za Watu wenye Ulemavu katika jamii na Haki za kiraia.

Kikanda, Sera ya Watu wenye Ulemavu ya Afrika Mashariki ya 2012 imeeleza mambo mbalimbali; na kimataifa haki hizo zimeanishwa kwenye Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu.

Tanzania imeridhia Mkataba huu. Baadhi ya Haki zilizoelezwa kwenye Mkataba huu ni usawa na kutokuwepo ubaguzi, haki ya kuishi, usawa mbele ya sheria, upatikanaji wa haki, kulinda utu wa mtu, uhuru wa kujieleza, kutoa maoni na kupata habari, haki ya faragha, kupata elimu na ajira pamoja na haki ya kushiriki katika siasa na maisha ya uongozi.

Mtazamo wa kuwa ulemavu ni ugonjwa ni tatizo kwasababu Watu wenye Ulemavu wenyewe hawawezi kuibadilisha jamii na jamii haitaweza kubadilika yenyewe ingawa jamii inahitaji kubadilika. Hivyo ni muhimu Watu wenye Ulemavu wakaonyesha wao wenyewe ni vitu gani hawawezi kufanya na ni mambo gani yanahitajika yafanyike ili kuwawezesha kufanya mambo wanayoweza kuyafanya wao wenyewe.

# Ijue Sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar Sheria Namb 8 ya, 2021



***Mkurugenzi Mipango, Sera na Utafiti Ofisi ya Makamu wa Kwanza Bi Daima M. Mkalimoto akimkabidhi cheti cha uhitimu wa mafunzo ya huduma masafa Mkurugenzi wa huduma masafa ndugu Abdulrahman A.Mani katika ukumbi wa Chuo cha Mafunzo yaliyoandaliwa na Jumuiya ya waliopata nafuu " Recovery Community "***

**SHERIA** ya kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar inatokana na dhamira ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi ya kusimamia kwa vitendo ibara ya 196 (a - g) ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 -2025. Ili kufanikisha azma hiyo ya mapambano, Serikali imeamua kuibadilisha Taasisi inayoshughulikia masuala ya dawa za kulevya ambayo ni Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya na kuwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar ambayo imepewa uwezo kamili wa kisheria wa kukabiliana kikamilifu na uhalifu huu wa Dawa za Kulevya ambao unaendelea kuathiri jamii nchini.

Madhumuni ya kufuta Sheria Namb. 9 ya 2009 ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya ni kutunga sheria mpya ya kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya itakayokuwa na uwezo wa kupeleleza, kukamata, kuchunguza na hatimaye kupeleka mahkamani mashauri yanayohusiana na dawa za kulevya pamoja na makosa mengine yanayofanana nayo.

Katika kukabiliana na janga hili Dk. Hussein Mwinyi, pale alipotimiza siku 100 za uongozi wake, aliazimia kufanya mageuzi makubwa kwenye juhudi za kudhibiti dawa za kulevya nchini. Azma hiyo ilitekelezwa, kama ilivyoelezwa awali, kwa kuifuta Sheria ya Udhibiti na Usafirishaji wa Dawa za Kulevya, Namba 9 ya mwaka 2009, na kutunga Sheria mpya inayokwenda sambamba na kasi ya sasa ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya na kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya yenye uwezo kamili wa kukabiliana na uhalifu huu.

Inafahamika kwamba, mabadiliko yanayotokea ulimwenguni katika wakati huu wa ukuaji wa sayansi na teknolojia yanatoa fursa pia kwa wahalifu wa dawa za kulevya kubuni mbinu mbadala za kujikinga na hatua zinazoweza kuchukuliwa dhidi yao. Maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano ya kimtandao yanaweza kutumiwa na wahalifu wa dawa za kulevya kuharibu ushahidi. Ukweli huu unalazimisha kuwepo kwa chombo imara na thabiti cha kusimamia udhibiti wa dawa za kulevya nchini ikiwa ni jitihada za kuunga mkono maazimio ya kikanda na kimataifa ili kuzinusuru nchi zisiendelee kuathriwa

***Inaendelea Uk. 21...***

*Inatoka Uk. 20*

na dawa za kulevya.

Bila shaka kuwepo kwa sheria hii ni muhimu kwani inapelekea kuwepo kwa Mamlaka yenye nguvu zaidi za kisheria na uwezo mkubwa katika kusimamia udhibiti wa dawa za kulevya nchini ambapo faida nyingi zitapatikana. Faida hizo ni kuwa na taasisi itakayokuwa na jukumu la kuchunguza, kukamata, kupeleleza na kufungua mashtaka mahakamani; Kuweko kwa usimamizi madhubuti katika kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya; na kutunza wenyewe vielelezo vya Dawa za Kulevya na kuepuka vielelezo hivyo kurudi kwenye jamii baada ya kesi ya msingi kumalizika.

Faida nyingine ni kupunguza na hatimae kuondoa kabisa makosa yanayohusiana na utumiaji na usafirishaji wa dawa za kulevya, hali itakayopelekea kupunguza na kuondoa athari zitokanazo na dawa za kulevya; kuimarika kwa nguvu kazi hasa vijana na hatimaye kukuza uchumi wa nchi; na kudhibiti matumizi ya dawa zinazotumika kwa matibabu ambazo zinaweza kutumika kama dawa za kulevya.

Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imegawika katika sehemu Kuu nane, na kujumuisha vifungu 86 vilivyozingatia masharti mbali mbali yanayohusiana na udhibiti wa matumizi na biashara ya dawa za kulevya. Kati ya hivyo, vifungu 26 ni makatazo juu ya mambo mbali mbali yanayohusu uhalifu wa dawa za kulevya na makosa yanayo fanana nayo.

Sehemu ya kwanza ya sheria hiyo inaelezea masharti ya awali ambayo yanajumuisha jina la sheria, kuanza kutumika na ufafanuzi wa maneno mbali mbali. Sehemu ya pili inaelezea uanzishwaji wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, uwezo wa Mamlaka, kazi za Mamlaka, uteuzi wa Kamishna Mkuu, sifa za Kamishna Mkuu, kazi za Kamishna Mkuu, wafanyakazi wa Mamlaka, wajibu wa kula kiapo cha utiifu kwa wafanyakazi wa Mamlaka, uwasilishaji wa ripoti ya hali ya dawa za kulevya, wajibu wa Serikali katika kuzuia dawa za kulevya, Kamati za Mikoa na kazi za Kamati za Mikoa.

Sehemu ya Tatu, inaelezea kuanzishwa Baraza la Taifa la Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, muundo, uwezo na majukumu ya Baraza. Kwa mujibu wa sheria hiyo, Kamishna Mkuu anakuwa Katibu wa Baraza na atakuwa na jukumu la utekelezaji wa maamuzi ya Baraza.

# Ijue Sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar Sheria Namb 8 ya, 2021

Sehemu ya Nne inahusiana na pendekezo la kuanzishwa kwa Mfuko, Usimamizi wa Mfuko na Hesabu na Ukaguzi za Mfuko. Sehemu ya Tano inaelezea makatazo ya kujihusisha na matumizi na biashara ya dawa za kulevya. Sheria inakataza mambo mbali mbali na kuweka adhabu kali kama ifuatavyo: -

Kulima bangi, mirungi, kumiliki, kusafirisha, kuuza na kununua mbegu zinazoweza kuzalisha dawa za kulevya adhabu yake ni kifungo cha maisha. Kufadhili biashara ya dawa za kulevya ambapo adhabu ya kosa hili ni kifungo cha maisha na kutaifisha mali zote zilizotokana na chumo la shughuli hiyo. Kusafirisha dawa za kulevya, kujihusisha kwa namna yoyote kinyume cha Sheria na kemikali zinazoweza kuzalisha dawa za kulevya ambapo adhabu yake ni kifungo cha Maisha.

Kumiliki mashine, vifaa na maabara kwa lengo la kutengeneza dawa za kulevya; kuruhusu jengo litumike kwa dawa za kulevya, mmiliki atatozwa faini isiyopungua milioni 10 au kifungo kisichopungua miaka 15 na kisichozidi miaka 30 au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Vile vile Sheria imetoa adhabu kwa mtu yeyote atakaekataa kutoa taarifa ama ushahidi unaohusiana na uhalifu wa dawa za kulevya au kutoa taarifa za uongo. Sheria imekataza kwa namna yoyote ile kusaidia au kusababisha kutendeka au kutenda uhalifu wa dawa za kulevya na kutoa adhabu sawa sawa na mtenda kosa mwenyewe. Sheria pia imekataza mtu yeyote kupanga au kushiriki katika kupanga kosa la dawa za kulevya na kuweka adhabu sawa na mtu aliyetenda kosa hata kama kosa lenyewe halikutendeka.

Sheria imeweka wajibu kwa mmiliki wa ardhi kutoa taarifa kwa Kamishna Mkuu kuhusu mazao haramu yaliyolimwa katika ardhi yake au shughuli yoyote haramu inayofanyika katika ardhi yake. Sheria imekataza mtu yeyote kuwa na mali zinazohusishwa au zinazotokana na chumo la uhalifu wa dawa za kulevya na ikithibitika fedha au chumo hilo litataifishwa.

Sheria imemkataza afisa yeyote kumtaja/kumfichua aliyempatia taarifa za uhalifu wa dawa za kulevya na akifanya hivyo adhabu ni faini isiyozidi shilingi milioni 15 au kifungo kisichopungua miaka 10 au vyote kwa pamoja. Aidha, sheria imeainisha makosa yasiyo na dhamana ambayo ni makosa yote ya dawa za kulevya. Masharti ya dhamana katika makosa ya dawa za kulevya yanaongozwa na sheria hii.

Katika kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya ni kosa kukutwa na kiwango kidogo cha dawa za kulevya kwa matumizi binafsi. Sheria imeipa uwezo serikali kuanzisha Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia kwa ajili ya kuwatambua, kuwatibu, kuwarekebisha tabia na kuwarejesha katika jamii watumiaji wa dawa za kulevya. Aidha, Sheria inakataza kutumia dawa za kulevya kwa namna yoyote. Pia ni kosa kukutwa katika eneo ambalo hutumiwa na watumiaji wa dawa za kulevya. Ni kosa vile vile kukutwa na vifaa vinavyosadikiwa kuwa vimetumika na dawa za kulevya kama vile sindano.

Sehemu ya Sita imeweka uwezo wa kufanya ukaguzi, upekuzi, kuzuia, kukamata, kuweka kizuizini na kuchunguza. Sehemu ya Saba imeweka uwezo wa kutaifisha mali au kitu kilichohusiana na kosa, katazo la kumiliki mali iliyopatikana isivyo halali, uwezo wa kufanya upelelezi au ukaguzi na kuzuia akaunti ya benki.

Sehemu ya Nane inazungumzia ufunguaji wa mashtaka ya makosa ya dawa za kulevya, kinga dhidi ya hatua zinazochukuliwa kwa nia njema, usafirishaji uliodhibitiwa kisheria, rufaa dhidi ya uamuzi wa Kamishna Mkuu, pamoja na dhamana itakayotolewa na mpinga rufaa.

# Kupunguza ulemavu unaosababishwa na ajali za barabarani na maradhi yasiyoambukiza



***Baraza la Watu wenye Ulemavu limetoa vifaa visaidizi zikiwemo baiskeli na fimbo nyeupe kwa Watu wenye Ulemavu.***

**AJALI** za barabarani ni tatizo kubwa la kiafya katika nchi zinazoendelea, ambapo barabara zimekuwa ni machinjio ya watu wengi. Ajali za barabarani zinapelekea watu kuweza kupata ulemavu na kwa wale watu ambao ni wenye ulemavu ajali hizo zinaweza kupelekea kupata ulemavu zaidi.

Sambamba na hilo, maradhi yasiyoambukiza yanajuilikana kama ni maradhi sugu, ambayo yanachukua muda mrefu hadi kubainika kwake ambayo yanatokana na mchanganyiko wa vitu mbali mbali ikiwemo fiziolojia, mazingira na athari za kimazingira.

Watu wa kila rika kitaifa, kikanda na kimataifa wameathirika na maradhi haya. Hali hii mara nyingi inachangiwa na kuwa na umri mkubwa, lakini ushahidi unaonyesha kuwa vifo vya zaidi ya watu milioni 15 vinavotokana na maradhi yasioambukiza yanatokana na kundi la wazee ambao wana umri kati ya miaka 30 hadi 69. Asilimia 85 ya vifo hivi inakisiwa kuwa, vinatokea katika nchi zenye kipato cha chini na zenye kipato cha kati.

Maradhi haya yanaweza kupelekea watu kupata ulemevu. Ulemavu pia unaweza kusababishwa na ajali za barabarani na kwa wale watu ambao tayari wana ulemavu ni dhahiri kuwa wanaweza kuongeza aina nyengine ya ulemavu mbali na ulemavu aliokuwa nao hapo kabla.

Taasisi zinazohusika na masuala ya usafiri iwe ni usafiri wa umma au wa binafsi ni vyema ikaandaa utaratibu wa kisheria wa kuwawekea mazingira rafiki Watu wenye Ulemavu katika nyanja ya usafiri wa barabarani.
Ni vyema taasisi hizo zikashauriana kwa pamoja na chombo cha Serikali kinachoshughulikia masuala ya Watu wenye Ulemavu hapa Zanzibar yaani Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu na taasisi nyengine zisizo za kiserikali.

Taasisi zitapaswa kufanya tathmini na kisha kutoa ushauri katika kuandaa mapendekezo au miongozo ya kuimarisha matumizi rafiki kwa watumiaji wote wa vyombo vya moto wakiwemo Watu wenye Ulemavu kwa manufaa ya kundi hili. Miongozo hiyo itaelekeza njia za kuwahakikishia abiria wanaosafiri wanakuwa salama muda wote wanapokuwepo barabarani.

Matukio na Ajali za barabarani Zanzibar
Kwa mujibu wa ripoti ya Jeshi la Polisi takwimu za makosa ya barabarani ya Tanzania ya mwaka 2020, kwa upande wa Zanzibar Mkoa unaoongoza kwa ajali za barabarani ni Mkoa wa Mjini Magharibi na Mkoa unaoongoza kwa makosa ya barabarani ni Kaskazini

***Inaendelea Uk. 11...***

# Kupunguza ulemavu unaosababishwa na ajali za barabarani na maradhi yasiyoambukiza



***Mkurugenzi wa Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu Mhandisi Ussi Khamis Debe akimkabidhi baiskeli ya maringi matatu Badali Mohamed Yussuf mkaazi wa Sebleni.***

***Inatoka Uk. 10***

Pemba.

Kuna hatua kadhaa zimechukuliwa na Jumuiya ya Usalama Barabarani kwa Watu wenye Ulemavu Zanzibar. Jumuiya hii imeweza kubuni alama sita zinazotumika kwa Watu wenye Ulemavu katika suala zima la kuhakikisha Usafiri salama kwa kundi hilo. Jumuiya hiyo mwaka 2019 ilitoa uelewa juu ya kutambulika kwa alama hizo sita. Katika mafunzo hayo jumla ya watu 1500 walishiriki.

Jumuiya pia kwa kwa kushirikiana na Jumuiya ya Usalama Barabarani kwa Watu wenye Ulemavu ya Tanzania Bara zimeweza kuzikagua baadhi ya alama zilizowekwa kwenye maeneo tofauti mjini na vijijini yakiwemo maeneo ya Mwanakwerekwe makaburini na maeneo ya njia ya Tunguu panapo mzunguko. Haya yote ni kwaajili ya kupunguza ajali za barabarani zinazoweza kupelekea kuongeza idadi ya wenye ulemavu nchini.

Dhana ya Usafiri salama barabarani ina lengo la kupunguza ajali za barabarani kwa Watu wenye Ulemavu na wasio na ulemavu; ajali ambazo zinazoweza kusababisha kupata ulemavu, ulemavu zaidi au kufariki kabisa.

Watumiaji wa barabara kama vile vyombo vya moto, vyombo vya magurudumu mawili, abiria, watembeao kwa miguu na watu watu wengine ndio wanaobeba dhana nzima ya usafiri salama. Usafiri salama umekuwa ndio kipaumbele kutokana na matukio kadhaa yanayojitokeza barabarani.

Kila mwaka watu wanakufa kutokana na kushindwa kuzingatia sheria za barabarani ipasavyo. Sababu zinazopelekea kutokea kwa ajali za barabarani ni nyingi. Sababu hizo ni pamoja na mwendo kasi, kuendesha bila kujali, kuendesha kwa kupita upande usio sahihi, kukipita chombo bila kuzingatia usalama, utumiaji wa simu wakati wa kuendesha gari, kuendesha chombo cha moto ukiwa dereva amelewa na kutokuzingatia ipasavyo alama za barabarani.

Kwa upande mwingine magonjwa yasiyoambukiza ni sababu kubwa ya vifo na ulemavu Ulimwenguni kote. Magonjwa makuu katika kundi hili ni pamoja na ugonjwa ya Moyo, ugonjwa ya mfumo wa hewa, Kisukari, na Saratani. Mengine ni pamoja na afya ya akili, figo, meno, magonjwa ya macho, masikio, na majeraha.




Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe Othman Masoud Othman akiwa na viongozi wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwenye sherehe za kutimiza mwaka mmoja akiwa madarakani zilizofanyika Golden Tulip ya Uwanja wa ndege, Zanzibar